More past papers are available on http://www.kenyaplex.com

Form 4 Mock 102/2 KISWAHILI Past Paper

Jina..................................................................................................Nambari.............................................

Shule
.......………………….........................................................Sahihi................................................
Tarehe................................................

102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI 2
JULAI / AGOSTI - 2010
MUDA: SAA 2 ½

TATHMINI LA PAMOJA WILAYA YA BUTERE – 2010
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E.)
102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI 2
JULAI / AGOSTI - 2010
MUDA: SAA 2 ½

MAAGIZO

1.Karatasi hili lina maswali manne. (Ufahamu, ufupisho, lugha na Isimu Jamii)
2.Jibu maswali yote kwenye nafasi zilizoachwa baada ya kila swali.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI

SWALIUPEOALAMA
115
215
340
410
Jumla80

Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa
Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa.
1.UFAHAMU (ALAMA 15)
Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.
“Sasa tumefika kwenye muskeli wangu“, alianza tena Mwanatenga. “Siku hiyo, Bwana Msa, baba’angu aliniita chumbani kwake, mimi na yeye tu peke yetu, na akaniweka kibao kuniaridhia hali yake ilivyo juu yangu“.

“E-eeng“, aliruka Bwana Msa, Najum alikazana juu ya kiti macho kayatoa. “Nd’oivo, Bwana Msa“, alijibu Mwanatenga na shingo kainyosha upande, uso na macho kumwelekeza, au kama anataka atokee mtu wa kutoa hoja za kukanusha yale aliyosema.

“Kaniaambia kwamba moyo wake umemili sana juu yangu na anataka kunioa, mambo kama hayo. Nilikaa tutwe, Bwana Msa, muda mzima na hata halafu yaliponitulikia vizuri maneno yake. Kwanza nilishtuka, moyo unan’enda shindo, nikawa na wasiwasi juu ya hali ya baba’ngu Bwana Wasiwasi. Wasiwasi ukazaa huzuni. Labda baba’ngu masikini kaharibika akili ghafla. Kwani, haiwezi kuwa yeye baba’ngu awe na fikira kama zile juu yangu, na yeye akawa bado mzima na akili yake timamu. Niseme nini, nijibu nini, nifanye nini?

“Lakini yeye mwenyewe baba’ngu aliponiona nimehamanika hivyo, na nimepigwa na butwaa, hapo hapo aliniweka sawa kwa kuniambia, “Sikiliza Mwanatenga, kama unafikiri kama miyendiye baba’ko fikira hiyo ondosha rohoni mwako. Wewe si mwanangu mimi, wala hunihuse be wala te. Mimi sina mtoto, lakinin n’na mali mengi sana. Sipendi kukuambia, lakini naona imenibidi. Basi wewe huna wazee. Mimi nimekuokota na wewe ungali mtoto mchanga umetupwa; na kwa huruma ukafika hapa ulipo. Basi, kwa hisani yangu, juu yako miaka yote hii, nakuomba utajamali kunipokea kuwa mumeo hivi sasa. Na wewe fikiri, nionavyo mimi, hiyo ndiyo njia pekee ya kukusaidia wewe kusetiri aibu iliyoandamana na wewe maisha yako kuhusu nasaba yako. Nikikuoa mimi, aibu yako itazibika, na wewe utakuwa Mwana wa Shimowazi na heshima kubwa kama hiyo“.

Bwana Msa alisikiliza yote hayo kwa tuo na mazingatio maakini, akawa anakwenda huku akirudi kule, kiko chake mdomoni kinatoa moshi tu.

“Endelea, mama“, alisema.

“Bwana Msa niliduwaa, nisiwe na la kusema“, Mwanatenga aliendelea. “Nilitaka nipate nafasi ya kufikiri mambo yake. Kwa mujibu wa maneno yake, posa zile ni za lazima, nikitaka nisitake“.

Posa zile zina matisho ya siri ndani yake, kama wasemavyo Waingereza ’Msumari (wa mdudu) uko mkiani kwake’ (hauko usoni). Kitisho cha maneno yale kimefichwa ndani yake kwa maneno ya

kutafuniatafunia.

’Tazama’, kasema. “- hiyo ndiyo njia ya pekee ya kusitiri aibu yangu, maana yake, njia nyingine yoyote...“
- Kama vile kukataa – itanitia fedhehani. Akaja akasema kuwa akinioa, nitakuwa mwana tena mwana bado wa shimowazi na heshima kubwa kama hiyo. Yaani kaniwekea njia kama sirati; nikiipita, nitafika peponi, nikishindwa kupita, nitaingia motoni.

“Yote hayo, Bwana.... Msa, yemenipitia moyoni mwangu kwa dakika ile ile. Hapo teana nilipandwa na hamaki, potelea mbali na liwe litakalokuwa“.

a) Taja aibu ya Mwanatenga aliyotaka kumwondoshea Bwana Wasiwasi.(alama 1)
……………………………………………………………………………………………..……
…………………………………………………………………………………………..………
b) Eleza hisia za msimulizi alipoelezwa na babake amwoe.(alama 3)
………………………………………………………………………………………………….
…………………………………………………………………………...…………………….
………………………………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………...………………………….
………………………………………………………………………………………………….
…………………………………………………………………………...…………………….
………………………………………………………………………………………………….
c) Kwa nini aibu ya Mwanatenga ingezibika kama angeolewa na Bw. Wasiwasi?(alama 1)
…………………………………………………………………………...…………………….
………………………………………………………………………………………………….
d) Hisani zipi Bw. Wasiwasi alimfanyia Mwanatenga?(alama 4)
……………………………………………………………………………………………..……
…………………………………………………………………………………………..………
……………………………………………………………………………………….…………
………………………………………………………………………………………..…………
………………………………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………...………………………….
………………………………………………………………………………………………….
…………………………………………………………………………...…………………….
………………………………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………...………………………….
………………………………………………………………………………………………….
…………………………………………………………………………...…………………….
………………………………………………………………………………………………….
e) “Kwa mujibu wa maneno yake, posa zile ni za lazima, nikitaka, nisitake“. Eleza jinsi posa hii ilivyokuwa ya lazima.(alama 2)

…………………………………………………………………………..……………………………..
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………...………………………..
…………………………………………………………………………………………………………
f) Msimulizi alipokuwa akisimulia kisa hiki walikuwa wangapi? Wataje.(alama 1)
…………………………………………………………………………...…………………………
…………………………………………………………………………………………………………
g) Eleza maana ya misemo hii kama ilivyotumiwa katika kifungu.(alama 3)
i) Akaniwekea kibao
…………………………………………………………………………...…………………………
…………………………………………………………………………………………………………
ii) Kaa tutwe
…………………………………………………………………………...………………………..
…………………………………………………………………………………………………………
iii) Kuisetiri aibu
…………………………………………………………………………...…………………………
…………………………………………………………………………………………………………

2.Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Sehemu muhimu ya elimu tamaduni ilikuwa ile ya maisha ya ndoa. Vijana, wake kwa waume, kwanza walifunzwa umuhimu wa kujiheshimu kimwili kabla ya kuolewa ama kuoa. Ilikuwa mwiko na aibu kwa msichana kupata mimba nyumbani, au kwa mvulana kumtunga mimba msichana kabla ya ndoa. Kwa hivyo shida ya watoto haramu haikuwepo katika jamii. Mafunzo kuhusu mpango wa uzazi yalikuwa muhimu. Ilikuwa ni aibu kwa mume na mkewe kuzaa watoto kabla ya miaka miwili au zaidi kupita. Wakati wa kunyonyesha mtoto mume na mke walitarajiwa kutoonana kimwili, nah ii ilisaidia katika kumlea mtoto.

Vijana wanaume kwa wake waliaswa kuhusu kuchagua wachumba wao kwa kuelezqa ni ukoo au mbari gani ingefaa kuoa au kuolewa nao. Ndoa zote zilihitaji vibali vya wazazi wa mume na mke. Haya yalipunguza shida za talaka kwenye jamii.

Vijana walifunzwa kuyaelewa mazingira yao, hasa kuhusu hali ya anga, ili wafahamu majira ya mvua na ukame. Walifunzwa kuchunguza na kufafanua hali za miti, ndege, nyota na wanyama wengine kujua ni majira gani ya hali ya hewa wanayotarajia ili kujiandaa nayo. Mafunzo ya hali ya hewa yaliwasaidia baadaye maishani katika shughuli za ukulima, ili waweze kutofautisha baina ya udongo wenye rutuba na ulio dhaifu, na pia waweze kujua mimea iliyoweza kumea katika aina mbalimbali za ardhi. Kutokana na mimea ya asilia mbalimbali, walijifunza ubora wa ardhi mbalimbali katika sehemu walizolima.

Elimu tamaduni haikuacha kuwafunza vijana jinsi ya kuyakabili magonjwa kati ya jamii. Kwa hivyo vijana wengine walikulia kuwa waganga waliotegemewa na jamii yao. Matibabu ya mitishamba

yalihitaji mafunzo mahususi yahusuyo kuitambua miti ifaayo kwa matibabu na matumizi katika kuponya magonjwa mbalimbali.

Elimu tamaduni ilitolewa na kufunzwa kwa dhati na watu waliofahamu mahitaji ya jamii yao vyema, kwa wakati ufaao na kwa vijana wa umri mbalimbali. Mambo muhimu ni kuwa elimu tamaduni ilisaadifu matakwa ya maisha ya jamii. Ilikuwa elimu ya maisha yake ya baadaye katika mazingira alimoishi.

Maswali

a)Eleza umuhimu wa elimu tamaduni katika jamii ya kale. (Maneno 70)(alm 8)

Matayarisho

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..……………………….
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..……………………….
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..……………………….
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..……………………….
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..……………………….
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..……………………….
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..……………………….
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..……………………….

Jibu

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..……………………….
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..……………………….
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..……………………….
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..……………………….
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..……………………….
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..……………………….

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

b)Eleza mambo muhimu yanayoshughulikiwa katika aya ya mwisho (maneno 30)

Matayarisho

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

Jibu

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..………………………

MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a)Tunga sentensi inayodhihirisha matumizi ya ngeli ya V – V(alm 1)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..………………………

b)Tambua mzizi katika neno kuadimika(alm1)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..………………………

c)Tunga sentensi moja ukitumia kiwakilishi cha pekee(alm1)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..………………………

d)Anidka kinyume cha(alm 2)

Kijakazi aliyepewa kazi na malkia alifurahi

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..………………………

e)Kanusha katika udogo(alm2)

Sisi tumemaliza kujenga nyumba ambayo ingekuwa yake angafurahi

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..………………………

f)Tambua sauti mbili zinazotamkiwa katika kaa-kaa ngumu(alm2)

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………...……………………….
g)Changanua sentensi ifuatayo ukitumia kielezo cha jedwali(alm4)
Gofu hushabikiwa na watu wachache sana.
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………...……………………….
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………...……………………….
h)Eleza matumizi ya 'ni' katika sentensi zifuatazo(alm3)
i)Wanasoka wanauchezea mpira uwanjani
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………...……………………….
ii)Kiptoo ni mkulima hodari
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………...……………………….
iii)Halima alinitembelea kwetu juzi
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………...……………………….
i)Bainisha shamirisho katika sentensi(alm2)
Mwalimu atawasimulia wanafunzi hadithi
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………...……………………….
j)Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo uliyopewa. (alm2)
i)Jua lilikuchwa msafiri akiwa njiani (tumia chwa katika kauli ya kutendewa)
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………...……………………….
ii)Mtoto alikunywa dawa aliyopewa na mama. (tumia nywa katika kauli ya kutendesha)
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………...……………………….
k)Bainisha virai katika sentensi zifuatazo(alm3)
i)Kwenye matope mengi gari hukwama
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………...……………………….
ii)Alishangilia mara kwa mara
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………...……………………….
iii)Leo asubuhi nilichelewa kuja kazini
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………...……………………….
l)Sahihisha(alm2)
Mtu mwenye anakula mkate ametumana aletewe chai
…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………..……………………….

m)Andika kwa msemo halisi(alm3)

Mwanasiasa aliwaambia wananchi kuwa hawakuwa na budi kuchangia maendeleo ya Sehemu yao

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………..……………………….

n)Akifisha(alm2)

Haya tuendelee ama tusiendelee mtangazaji aliuliza

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………..……………………….

o)Eleza miingiliano ya kisarufi ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo(alm2)

Yohana alituenzi baada ya sisi kumtatulia shida zake enzi hizi za uwajibikaji

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………..……………………….

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………..……………………….

p)Andika upya kwa kutumia O' rejeshi tamati(alm2)

Mtu ambaye hufungwa jela ni yule ambaye huhalifu sheria

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………..……………………….

q)i)Sentensi changamano ni gani?(alm1)

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………..……………………….

ii)Tunga sentensi moja changamano

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………..……………………….

r)Tumia maneno kwenye ujozi ifuatayo kudhihirisha maana tofauti katika sentensi(alm2)

Suka / zuka

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………..……………………….

s)Unda nomino mbili kutokana na kitenzi(alm2)

Komboa

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………..……………………….

ISIMU – JAMII

Eleza sifa tano za lugha ya magazeti(alm10)

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………..……………………….